

HALMASHAURI YA MJI KONDOA



MUHT. BZA. NA 1/09/11/2021

MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 09/11/2021 KATIKA UKUMBI WA BIASHARA WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA.

WALIOHUDHURIA:

- | | | |
|--------------------|---|-----------------|
| 1. Hassan Mtamba | - | Mwenyekiti |
| 2. Hassan Kisseto | - | Mjumbe |
| 3. Lucy Timba | - | Mjumbe |
| 4. Monica Kimaro | - | Mjumbe |
| 5. Shabani N. Sued | - | Mshauri wa Bodi |
| 6. Mussa Kimwaga | - | Katibu |

WASIOHUDHURI

- | | | |
|------------------|---|-------------|
| Dr Nelson Bukulu | - | Kwa taarifa |
|------------------|---|-------------|

Sekretarieti

- | | | |
|-------------------|---|-----------|
| Vivian M. Leskana | - | Mwandishi |
|-------------------|---|-----------|

MUHT. BZA .NA.1/04/11/2021/01 - KUFUNGUA KIKAO.

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 4:05 Asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe wote na kuomba ushirikiano wao wa kujadili agenda zilizowasilishwa na kuweza kutolea maamuzi

MUHT. BZA.NA. 1/04/11/2020/02 – KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO

Agenda zifuatazo zilithibitishwa na wajumbe na zilikubaliwa kujadiliwa

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda za kikao

3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 19/08/2021
4. Kupitia manunuzi yaliyofanyika kwa waraka wa maoni (circular resolution)
5. Kupitia taarifa ya manunuzi ya robo ya kwanza
6. Kuridhia njia ya manunuzi ya kazi za ujenzi madarasa kwa shule za Msingi Sekondari, Nyumba ya watumishi Kituo cha Afya Serya na jengo la dharura(EMD) Hospitali ya Halmashauri ya KOndoa Mji kupita fedha za UVIKO-19
7. Mengineyo
8. Kufunga Kikao

MUHT: BZA.NA. 1/04/11/2021/03 - KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA CHA TAREHE 19/08/2021

Baada ya kusomwa na kutokuwa ma masahihisho muhtasari wa kikao cha tarehe 19/08/2021 ulithibitishwa na kusainiwa

MUHT: BZA.NA. 1/04/11/2021/04 - KUPITIA MANUNUZI YALIYOFANYIKA KWA WARAKA WA MAONI (CIRCULAR RESOLUTION) KWA KIPINDI CHA ROBO YA NNE 2020/2021

Katibu aliwasilisha kwa kusoma manunuzi yaliyofanyika kwa waraka wa maoni (Circular resolution yenye jumla ya Tsh 71,261,634.00 kwa ajili ya kujadiliwa na kuridhiwa.

Wajumbe walipitia na kuridhia manunuzi hayo yaliyofanyika kwa circular Resolution yenye jumla ya Tsh 71,261,634.00, aidha orodha ya manunuzi hayo uliwasilishwa

MUH: BZA.NA. 5/04/11/2021/05 - KUPITIA TAARIFA YA MANUNUZI YA ROBO YA KWANZA

Katibu aliwasilisha taarifa ya manunuzi ya kipindi cha robo ya pili 2020/2021.

Wajumbe walijadili na kuiridhia taarifa hiyo ya manunuzi ya robo ya pili kwa mwaka 2020/2021 yenye jumla ya Shilingi 75,542,834.00 kwa ajili ya manunuzi ya vifaa na huduma zisizo za kitaalamu, mchanganuo uliwasilishwa.

MUHT: BZA.NA. 1/04/11/2021/06 Kuridhia njia ya manunuzi ya kazi za ujenzi madarasa kwa shule za msingi na sekondari kupita fedha za UVIKO na TOZO Katibu aliwasilisha maombi ya kuridhia njia ya manunuzi ya FORCE ACCOUNT kwa fedha zilizopelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo kwa mchanganuo ufuatao

- Ujenzi wa madarasa kwa shule za Msingi na Sekondari jumla ya kiasi cha Shilingi 460,000,000.00
- Ujenzi wa Jengo la Dharura katika hospitali ya Halmashauri ya Kondo Mji Kiasi cha Shilingi 300,000,000.00
- Ujenzi wa nyumba ya watumishi kituo kipya cha afya cha Serya kiasi cha Shilingi 90,000,000.00

Wajumbe walijadili manunuzi hayo na kuridhia yafanyike kwa njia ya force Account,


MUHT: BZA.NA. 1/04/11/2021/07 MENGINEYO

- Wajumbe waliendelea kusesitiza kuwa kikao cha Bodi ya Zabuni ni kikao cha kisheria hivyo Mkurugenzi ashauriwe kufanya malipo, aidha Mwenyekiti na Katibu waende kwa Mkurugenzi kwa mara nyingine kwa ajili ya ufatiliaji wa posho hizo.
- Makabrasha ya kikao cha Bodi yawasilishe mapema kwa wajumbe ili waweze kupata muda wa kuyapitia ilikurahisha kikao.

MUHT: BZA.NA. 1/17/7/2020/08 - KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango na ushirikiano wao kwenye kikao na alifunga kikao mnamo saa 5:54 Asubuhi

Umethibitishwa Na:


.....
Katibu

Tarehe... 04/11/2021


.....
Mwenyekiti